

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**  
*(Barua zote zielekezwe Kwa Mkurugenzi wa Halmashauri)*

☎ Simu: Na : 026 -2702647  
☎ Faksi Na : 026 - 2702203



Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa,  
S.L.P 162,  
**IRINGA.**

---

**Kumb. Na. IMC/S.20/2/VOL.I/112**

**Tarehe 3/11/2020**

# **TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI**


Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa anapenda kuwataarifu waombaji kazi waliotuma maombi ya kujaza nafasi wazi zilizotangazwa na Halmashauri, kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe **18/11/2020** hadi **19/11/2020** katika **UKUMBI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA** na hatimaye kuwapangia vituo vya kazi waombaji kazi watakaofaulu usaili huo.

Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo;-

- i. Usaili utafanyika kuanzia tarehe **18/11/2020** hadi **19/11/2020** kama ilivyoainishwa kwenye tangazo hili.
- ii. Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi.
- iii. Vitambulisho vinavyokubalika ni Pamoja na Kitambulisho cha Mpiga Kura, Kitambulisho cha uraia au Hati ya kusafiria.
- iv. Wasailiwa wanatakiwa kufika na VYETI VYAO HALISI, kuanzia cheti cha kuzaliwa, Cheti cha Kidato cha IV, VI, astashahada na kuendelea kutegemea na sifa za mwombaji.

- v. Wasailiwa watakaowasilisha "Testimonials", "Provisional Results", Statement of Results slips) HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.
- vi. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula. Usafiri na malazi.
- vii. Kila msailiwa azingatie tarehe na mahali alipopangiwa kufanyia usaili.
- viii. Kwa woambaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA).
- ix. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo, hivyo wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya Tangazo husika.

MKURUGENZI WA MANISPAA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA,  
S.L.P. 162,  
**IRINGA.**



*HAMID A. NJOVU*  
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI**  
**MANISPAA YA IRINGA**  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
IRINGA